**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)**

**MTIHANI WA UTAMILIFU KIDATO CHA PILI 2024 KANDA YA NYANDA ZA JUU KUSINI**

**KISWAHILI**

**MUDA: SAA 2:30**

**MAELEKEZO**

i) Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali 10
ii) Jibu maswali yote kwa umakini na ufasaha katika sehemu zote
iii) Andika namba yako ya mtihani katika kila ukurasa wa karatasi ya kujibia uliyotumia
iv) Majibu yote yaandikwe kwa kalamu ya bluu au nyeusi
v) Simu za mkononi hazirusiwi ndani ya chumba cha mtihani

**SEHEMU A (Alama 15)**

1. Chagua herufi ya jibu sahihi katika vipengele (i) hadi (x) kisha andika herufi ya jibu sahihi hilo katika kisanduku ulichowekewa mwishoni mwa swali lote

i) Shule zetu zimeweka mikakati kabambe ya kutokomeza daraja la pili **ili** zibaki na daraja la kwanza pekee. Neno ili katika lugha hii ni aina gani neno?
a) Kiunganishi
b) Kivumishi
c) Kielezi
d) Kihusishi

ii) Mwalimu aliwaagiza wanafunzi wawili wajibizane mbele ya wanafunzi wenzao darasani. Ni kipera gani kinawakilisha walichofanya wanafunzi hao?
a) Ngonjera
b) Majigambo
c) Kichekesho
d) Igizo

iii) Sauti ya lugha inayotamkwa bila kuwapo kwa kizuizi chiochote kwenye mkondo wa hewa huitwaje?
a) Mkazo
b) Konsonati
c) Irabu
d) Silabi

iv) Ni kauli ipi inayotumika katika uundaji wa neno ‘’nitamfitinisha’’
a) Kutendeana
b) Kutendesha
c) Kutenda
d) Kutendea

v) Maumbo yanayoungana kuunda neno huitwa mofimu ilihali maana zizlizosetiriwa ndani ya mofu huitwa mofimu. Je kati ya maneno yafuatayo ni lipi limeundwa na mofu au mofimu tegemezi ?

a) Shangazi
b) Ugali
c) Ngoma
d) Mjomba

vi) Tangu zamani Mussa alikuwa mwizi. Alikanywa lakini hakusikia. Siku moja aliingia benki ili kuiba fedha. Mlinzi alimuona na kumpiga risasi ya mguuni. Kimoyomoyo Mussa akajisemea '' asiyesiki la mkuu huvunjika guu''. Maelezo yaliyopigiwa mstari hutumika kwenye kipera gani cha hadithi kama msingi wa kutunza jamii?
a) Soga
b) Ngano
c) Vigano
d) Tarihi

vii) Rafiki na Kazi ni watoto wa bwana barua. Kazi ana wajukuu kumi na mbili ambao ni muhimu kuzingatia unapowataja. Je, rafiki ana watoto wangapi ambao unapowataja lazima uwazingatie?
a) Saba
b) Kumi na moja
c) Sita
d) Wanne

viii) ''**Pigia''** Anna alitamka neno hilo alipokaribishwa kuwasilisha risala kwa mgeni rasmi. Mgeni rasmi aliposikia neno hilo alipata utata. Je, nikiambishi gani kilichomfanya mgeni rasmi kupata utata waneno hilo?
a) - i -
b) Pig -
c) - a -
d) - ia –

ix) Juma alikuwa akitaniana na Mathayo ''Juma akamwambia Mathayo ni mnene kama pipa'' na Mathayo akamwambia Juma ni ''mwembamba mithili ya sindano''. Je, Juma na Mathayo walitumia tamathali gani ya semi?
a) Tanakali sauti
b) Tashibiha
c) Sitiari
d) Tashihisi

x) Kija alimsihi shangazi Yembe awasaidie kulipa ada ya Maisara ili aendelee na masomo yake. Shangazi aliwapa kisogo kauli iliyopigiwa mstari ina maana gani?
a) Aliwapuuza
b) Aliwaitikia
c) Aliwasikiliza
d) Alikubaliana nao

| i | ii | iii | iv | v | vi | vii | viii | ix | x |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | |

2. Oanisha dhana za maneno kutoka fungua 'A' na maneno yaliyopo fungu 'B' ili kuunda dhana kamili kisha andika herufi ya jibu sahihi kwenye kisanduku ulichopewa.

| Orodha A | | Orodha B | |
|---|---|---|---|
| i. | Kipindi cha kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa 1992-1995 | A. | Wafanyakazi hewa |
| ii. | Kipindi cha awamu ya tano | B. | Mchumia tumbo |
| iii. | Kipindi cha vita ya Kagera 1978-1979 | C. | Unga wa yanga |
| iv. | Kipindi cha njaa kali ya mwaka 1974-1975 | D. | Vitakasa mikono |
| v. | Kipindi cha UVIKO 19 | E. | Ulanguzi |
| | | F. | Ngangari |
| | | G. | Disco |
| | | H. | Nduli |
| | | I. | Uhuru na umoja |
| | | J. | Uhuru na kazi. |

| i | ii | iii | iv | v |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |

**SEHEMU B (Alama 70)**

3. Katika kazi ya fasihi simulizi viungo vya mwili kama vile macho, mdomo, kichwa, miguu hata mikono husaidia kufanikisha kazi hiyo na kufikisha ujumbe kwa jamii. Taja na eleza kwa ufupi faida tano za kutumia viungo hivyo vya mwili vilivyotajwa hapo juu katika kazi ya fasihi simulizi.

a) ______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________

b) ______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________

c) ______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________

d) ______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________

e) ______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________

4. a) Eleza mambo makuu matano yanayotakiwa kuzingatiwa na mzungumzaji katika kuteua maneno na muundo wa tungo.

i) ______________________________________________
______________________________________________

ii) ______________________________________________
______________________________________________

iii) ______________________________________________
______________________________________________

iv) ______________________________________________________________________
______________________________________________________________________

v) ______________________________________________________________________
______________________________________________________________________

b) Eleza njia zinazotumika kuunda misimu ifuatayo

i) Demu ______________________________________________________________________

ii) Kuzimikia ______________________________________________________________________

iii) Disco ______________________________________________________________________

iv) Ferouz ni twiga ______________________________________________________________________

v.Mataputapu ______________________________________________________________________

5. A) Kwa kila mzizi uliopewa hapa chini unda nomino mbili kutokana na mzizi huo.

| | | | |
|---|---|---|---|
| i) | –f— | (a)____________________ | (b)____________________ |
| ii) | ---sem--- | (a)____________________ | (b)____________________ |
| iii) | ---nyw--- | (a)____________________ | (b)____________________ |
| iv) | ---L--- | (a)____________________ | (b)____________________ |
| v) | ---pig— | (a)____________________ | (b)____________________ |

b) Eleza kazi moja ya mofimu tegemezi iliyopigiwa mstari katika maneno yafuatayo.

i) <u>Ha</u>wachezi ______________________________________________________________________

ii)<u>Tu</u>nasoma ______________________________________________________________________

iii) A<u>ta</u>cheza ______________________________________________________________________

iv) Ali<u>ye</u>pika ______________________________________________________________________

v) <u>Hu</u>andika ______________________________________________________________________

6. A) Rafiki yako amepewakazi na mwalimu wake wa Kiswahili, akusanye kazi mbalimbali za fasihi simulizi kutoka katika jamii za kitanzania lakini ameshindwa na kusema hajui namna ya kuzipata. Kwa kutumia ujuzi wako wa somo la Kiswahili mueleze rafiki yako njia tano za kukusanya kazi za fasihi hiyo.

i) ______________________________________________________________________

ii) ______________________________________________________________________

iii) ______________________________________________________________________

iv) ______________________________________________________________________

v) ______________________________________________________________________

B) Fasihi simulizi ndio fasihi ya awali iliyoanza wakati binadamu alipoanza kutumia lugha. Mara kwa mara ilipowasilishwa kwa hadhira ilichukua nduni muhimu kadha ambazo sio rahisi kuziona katika fasihi andishi. Taja na fafanua nduni tano.

i) ______________________________________________________________________

ii)______________________________________________________________________

iii)_____________________________________________________________________

iv)_____________________________________________________________________

v.______________________________________________________________________

7. Soma utungo ufuatao kisha jibu maswali yanayofuata.

Mwanaukale: Sikia mwanausasa, usije haribikiwa,
Kuleta zako siasa, usije changanyikiwa,
Dada yako nakuasa, naona umevamiwa,
Utandawazi mkasa, kwa kisa cha maadili.

Mwanausasa: Na wewe mwanaukale, uache kunivuruga,
Sinipigie kelele, kunitoa kwenye uga,
Acha nipige misele, mtandaoni jimwaga,
Kuna burudani tele, huziwezi hizi swaga.

Mwanaukale: Ndugu acha ujeuri, nasaha zangu kariri,
Kishushe chako kiburi, sikiliza ushauri,
Wajichimbia kaburi, kwa kuzidisha kiburi,
Utandawazi ni janga,  kwa maadili nchini.

Mwanausasa: Dada yangu mwanaukale, acha kupiga kelele,
Acha ushamba milele, kama vipi kalale,
Huku kuna raha tele, kwetu tujuayo yale,
Natetema ka'Mayele, shangwe na vigelegele.

Mwanaukale: Huoni yake madhara, kukesha mtandaoni,
Kazi zote za dolola, hata kula huthamini,
Wajitia ufukara, pesa zaisha bandoni,
Kutwa kujipiga picha, na kuchat na wahuni.

Mwanausasa: Chakula usichokila, hujui utamu wake,
Wewe endelea kulala, ajuza asomakeke,
Utandawazi chakula, kwa raha swaga zake,
Hata unambie nini, mtandaoni sing'oki.

Utandawazi: Kwani kuna shida gani? Mbona ndugu mwagombana,
Hebu kwanza tulieni, msije mkashikana,
Sasa hebu nelezeni, tupate kuelewana,
Mesikia natajwa, kwa wema na ubaya,

Mwanausasa: Afadhali umekuja, upate tusaidia,
Dada yangu anakutaja, lakini na mimi pia,
Mimi najua wewe unatija, dadangu akuchukia sasa,
Tuweke bayana, zifaazo tuweze tulia.

Mwanaukale: Tena wewe mjaa laana, nimekutafuta sana!,
Wawaharibu vijana, kwa mambo yaso na maana,
Dunia umeibana, wapotosha ya maana.
Mimi ninakuchukia, sioni ya kwako tija,

Utandawazi: Sasa nisikilizeni, sifa zangu niwapeni,
Mimi ni mtu makini, wala siwapotosheni,
Mambo yote mesheheni, mema mabaya kapuni
Faida au hasara, huo uchaguzi wako.

**MASWALI**

(i) Utungo huo unaitwaje.
..........................................................................................................................

(ii) Eleza kwa muhtasari kichwa kisichozidi maneno matano.
..........................................................................................................................

(iii) Bainisha mbinu mbili za kishairi zilizotumika katika utungo huu.
..........................................................................................................................

(iv) Eleza uhusiano uliopo baina ya wahusika wanaobishana juu ya utungo huu.

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

(v) Fupisha maudhui ya utungo huo kwa maneno yasiyopungua 70 na yasiyozidi 75

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

.

8. (a) Kwa kutumia mifano fafanua dhima zifuatazo za rejesta

(i) Kuficha jambo kwa wasiohusika.

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

(ii) Rejesta husaidia kukuza lugha

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

(iii) Rejesta hutumika kama kitambulisho cha jamii.

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

(iv) Rejesta hutumika kurahisisha mawasiliano.

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

(v) Rejesta hutumika kupamba lugha.

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

(b) Desderia alikuwa hana uelewa mzuri kuhusu neno utata, Happy akamueleza kuwa utata ni haki ya neno au sentensi kuwa na maana zaidi ya moja. Wewe kama Happy mfafanulie Desderia kwa kutumia maneno yafuatayo

i. Kaka (maana 3)

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

.......................................................................................................

ii. Mgeni (maana 2)

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

9. Rafiki yako hakuwepo darasani wakati mwalimu wa Kiswahili alipokuwa anafundisha mada ya uandishi wa barua pepe. Mbainishie rafiki yako vipengele vitano vya msingi anavyopaswa kuvizingatia wakati wa kuandika ujumbe wa barua pepe

i. ......................................................................................................

ii. ..........................................................................................................

iii. ..........................................................................................................

iv. ..........................................................................................................

v. ..........................................................................................................

10. Baraza la Kiswahili laTaifa (BAKITA) linapenda kuwatangazia fursa ya ufundishaji wa lugha ya kiswahili kwa wageni kwa wataalamu wote waliohitimu shahada ya Kiswahili kutoka katika taasisi za taaluma ya Kiswahili katika vyuo vikuu vinavyotambulika na serikali nchini. Maombi yatumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Baraza, S.L.P 5440 Dar es salaam kupitia kwa Mkuu wa idara ya mafunzo ya lugha kwa wageni wa baraza hilo na nakala ya barua hiyo itumwe kwa mkuu wa idara ya maendeleo ya Lugha na utamaduni katika Wizara ya Habari,Utamaduni,Sanaa na Michezo Tanzania,S.L.P 745 Dar es salaam. Mwisho wa kutuma maombi hayo ni tarehe 20 mei 2024. Wewe ukiwa ni miongoni mwa wenye sifa hitajika changamkia fursa hiyo, jina lako ni Nakipenda Kiswahili, S.L.P 2950 Morogoro